



## **TAARIFA YA MKUTANO WA 46 WA WANAHISA**

### **TAARIFA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa arobaini na sita (46) wa Wanahisa wa Tanzania Breweries Limited utafanyika tarehe 5 Mwezi Septemba, 2019 katika hoteli ya iHyatt Regency - The Kilimanjaro (Kibo Ballroom) barabara ya Kivukoni Jijini Dar es Salaam kuanzia saa nne kamili asubuhi.

#### **AGENDA ZA MKUTANO:**

1. Taarifa ya Mkutano
2. Kupitia kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita
4. Kupitia na kuidhinisha taarifa ya Mahesabu na Ripoti ya Wakurugenzi kwa Mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2018
5. Kuthibitisha gawio lililolipwa kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2018
6. Kuteua Kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama Wakaguzi wa nje wa Mahesabu kwa Mwaka utakaoishia 31 Desemba 2019
7. Mengineyo

Mwanahisa ambaye atashindwa kuhudhuria anaweza kujaza fomu ya uwakilishi na kuteua Mwakilishi anayemtaka. Mwakilishi huyo atakuwa na haki ya kupiga kura na si lazima awe Mwanahisa.

Fomu za uwakilishi zitumwe kwa Katibu wa Kampuni angalau masaa 48 kabla ya Mkutano. Mwanachama atakayehudhuria ni lazima aje na cheti cha hisa au stakabadhi ya CDS pamoja na kitambulisho chake.

#### **KWA NIABA YA BODI YA WAKURUGENZI KATIBU WA KAMPUNI**

Angalizo:

- i. Mwanahisa ambaye anataka kuleta azimio atoe taarifa ya azimio kabla ya tarehe 30 Agosti, 2019.
- ii. Wanahisa watajigharamia gharama za kuhudhuria Mkutano.

#### **NYARAKA:**

**Kumbukumbu za kikao kilichopita pamoja na Taarifa ya Hesabu zinapatikana katika tovuti ya <https://tblannualreports.co.tz/>**

**Kwa taarifa au ufafanuzi zaidi tafadhari tuma barua pepe kwa;  
[TBLCorporate.communications@tz.sabmiller.com](mailto:TBLCorporate.communications@tz.sabmiller.com)**